Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

HEKIMA NI UHURU

HEET
HIGHER EDUCATION FOR ECONOMIC TRANSFORMATION

Toleo la 06

# Jarida la HEET UDSM

Toleo la Agosti - Oktoba 2024

HEET
Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi



Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo wakiwa na baadhi ya viongozi na wafanyakazi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wakati Kamati ilipotembelea Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili kufahamu kuhusu utekelezaji wa Mradi wa HEET, hivi karibuni.




## Ndani ya Jarida hili...


**Bunge lakipongeza Chuo** katika Utekelezaji wa Mradi wa HEET 6

**Mapitio ya Mitaala UDSM** yafanyika kwa mafanikio 14

**Ujenzi wa Majengo ya Mradi** wa HEET UDSM Kukamilika kwa Wakati 18

**Kampasi mpya ya UDSM yachochea** uwekezaji Mkoa wa Kagera 22

**UDSM chapongezwa kwa kuzindua** kamati za KASEMA katika maeneo ya Mradi wa HEET 24








# YALIYOMO


| | |
|---|---|
| 3 | Ujumbe wa  Makamu Mkuu wa Chuo |
| 4 | Ujumbe wa Mratibu |
| 5 | UDSM chakabidhi maeneo ya HEET kwa wakandarasi kwa ajili ya Ujenzi |
| 6 | Bunge lakipongeza Chuo katika Utekelezaji wa Mradi wa HEET |
| 8 | Mpango wa pili wa uambatishaji wa wafanyakazi wazinduliwa kwa ari kubwa |
| 9 | Mpango wa pili wa uambatishaji wa wafanyakazi wazinduliwa kwa ari kubwa |
| 10 | Ujumbe wa Naibu Mratibu |
| 11 | Tahariri |
| 12 | Matukio katika Picha |
| 14 | Mapitio ya Mitaala UDSM yafanyika kwa mafanikio |
| 16 | Mapitio ya mitaala yazingatia mbinu bunifu na mafunzo ya ziara ya ulinganishi viwango |
| 18 | Ujenzi wa Majengo ya Mradi wa HEET UDSM Kukamilika kwa Wakati |
| 20 | UDSM chatoa mafunzo kuhusu Ukatili wa Kijinsia kwa watoa huduma katika maeneo ya HEET |
| 21 | Jitihada madhubuti za kukuza mazingira yasiyo na ukatili wa kijinsia UDSM zapamba moto |
| 22 | Kampasi mpya ya UDSM yachochea uwekezaji Mkoa wa Kagera |
| 24 | UDSM chapongezwa kwa kuzindua kamati za KASEMA katika maeneo ya Mradi wa HEET |
| 25 | Wanufaika wengine watatu wa Ufadhili wa HEET UDSM wahitimu Masomo ya Umahiri |

# Ujumbe wa Makamu Mkuu wa Chuo

**Prof. William A. L. Anangisye**

**Makamu Mkuu wa Chuo**



Kwa niaba ya Menejimenti ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ninatumia fursa hii kuwakaribisha wasomaji wetu katika Toleo la Sita la Jarida la HEET-UDSM. Kama ilivyo ada, Chuo kinaendelea kuwajulisha wadau wake kuhusu utelekezaji wa Mradi wa HEET tangu ilipotolewa taarifa ya utekelezaji katika awamu iliyopita ambayo ilikuwa Juni 2024.

Lengo ni kuwafanya wadau wetu kupata taarifa kuhusu utelezaji wa shughuli mbalimbali katika mradi huu wa kimkakati. Usimamizi na utoaji wa taarifa kuhusu utekelezaji wa Mradi wa HEET ni suala muhimu kwani ni sehemu ya utekelezaji wa mpango mkakati wa Chuo ambao nao unazingatia vipaumbele vya kimkakati vya Taifa.

Tunapenda kuwajulisha kwamba Chuo kimeendelea na usimamizi na tathmini ya Mradi ili kuhakikisha kwamba kunakuwa na manufaa katika utekelezaji wa malengo ya mradi. Kuanzia ripoti iliyotolewa katika toleo lililopita, Chuo kimechukua hatua mbalimbali za kimkakati ambazo zimekuwa na matokeo chanya katika kufanikisha malengo ya mradi.

Wakati ambapo Utekelezaji wa Mradi unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 23 kuanzia ulipoanza kutekelezwa mwezi Julai 2022, asilimia 72 ya bajeti imekwishatengwa kwa ajili Utekelezaji wa Mradi kwa awamu husika. Hili limefanyika baada maeneo 11 ya ujenzi kupata wakandarasi kuanzia mwezi Juni 2024. Menejimenti ya Chuo imedhamiria kuhakikisha kwamba wakandarasi wote wanakamilisha kazi zao kabla au ifikapo mwezi Novemba 2025.

Mameneja wetu wa wakandarasi kupitia Kitengo cha Utekelezaji wa Mradi wanasimamia kwa karibu shughuli mbalimbali zilizo katika mkataba katika maeneo yote ya mradi. Ni matarajio yetu kwamba washauri wa mradi wataendelea kuwasimamia wakandarasi na kukishauri Chuo ili kuhakikisha kwamba mradi unakamilika kwa ufanisi na kwa wakati.

Maendeleo yaliyofikiwa katika uboreshaji wa mitaala kwa kuzingatia mbinu bunifu za ufundishaji ni ya kuridhisha na kwamba kufikia Novemba 2025 Chuo kitaanza utekelezaji wa programu zilizoboreshwa. Chuo kimeendelea kuimarisha ushirikiano na tasnia mbalimbali kwa kutia saini mikataba mipya ya maridhiano, kuendelea na utekelezaji wa mikataba iliyokuwepo, na kupeleka zaidi watumishi katika asasi mbalimbali ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mikataba iliyoridhiwa.

Ninatumia fursa hii kuishukuru Kamati ya Bunge inayohusika na masuala ya elimu, utamaduni na michezo kwa ushauri na maelekezo waliyotupatia wakati wa ziara yao iliyolenga kukagua utekelezaji wa Mradi wa HEET-UDSM. Menejimeti ya Chuo itazingatia ushauri na maelekezo yote yaliyotolewa na kamati ili kufanikisha utekelezaji wa Mradi.

Tunatoa shukrani za dhati kwa viongozi wa mikoa na serikali za mitaa ambapo Mradi wa HEET unatekelezwa kwa ushirikiano wanaoutoa kwa wakandarasi wetu. Aidha, ninatumia fursa hii kuwashukuru wadau wote ambao wameendelea kutuunga mkono katika utekelezaji wa Mradi wa HEET katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Chuo kinatambua mchango kinaoupata kutoka katika Serikali, Benki ya Dunia, katika jamii na kwa wanahabari. Tunathamini mchango tulioupata kutoka kwa wadau wengine katika Utekelezaji wa Mradi wa HEET ikizingatiwa kwamba utekezaji wa mradi wetu umefanyika kwa kuzingatia mafunzo tuliyoyapata kutoka kwa wengine. Wazabuni, washauri wa kitaalamu na wakandarasi wanastahili pongezi kwa kujitoa kwao kiuwajibikaji na kitaalamu.

Kwa mara nyingine ninakukaribisheni wasomaji wetu nikiamini kwamba mtalifurahia Jarida hili.

# *Ujumbe wa Mratibu*



## Prof. Bernadeta Killian

### Ujumbe wa Mratibu HEET - UDSM

Karibuni sana wasomaji wetu katika Toleo la Sita la Jarida la HEET-UDSM. Katika toleo hili, mbali na mambo mengine, tunapenda kuwajulisha kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Mradi wa HEET katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Shughuli hizi zimepangwa katika maeneo matano ya kipaumbele ambayo ni Uhandisi na Teknolojia, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Kilimo na Kilimobiashara, Uhandisi wa Maendeleo ya Mji na Mazingira na Uchumi.

Miongoni mwa mafanikio makubwa yaliyofikiwa ni maendeleo ya miundombinu ambayo iko katika hatua ya ujenzi. Kusainiwa kwa mkataba kwa ajili ya ukarabati wa majengo Dar es Salaam na ujenzi wa majengo mapya katika mikoa ya Dar es Salaam, Lindi na Buyu, Zanzibar mwezi Februari 2024 kumefungua njia ya kuanza kwa ujenzi kuanzia mwezi Aprili 2024. Maendeleo ya miradi yanajidhihirisha ambapo ujenzi katika maeneo mengi umekamilika katika sehemu ya msingi. Wakati huohuo wakandarasi wamefika eneo la ujenzi na ujenzi unaendelea katika kampasi ya Kagera baada ya kusainiwa kwa mkataba wa ujenzi tarehe 17 Mei 2024.

Kwa upande wa mapitio ya mitaala, Chuo kimefanikiwa kupitia programu 94 (38 za shahada za awali na 56 za uzamili) ambapo programu hizi zimepitiwa na Kamati ya Kiufundi ya Seneti na ile ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Tekolojia kwa ajili ya kupitishwa na Seneti na kupata ithibati kutoka Tume ya Vyuo Vikuu (TCU). Katika eneo hili Chuo kimevuka malengo yake iliyojiwekea wakati wa kuanza kwa Mradi huu ya kupitia programu 60. Mapitio ya mitaala yamezingatia ripoti ya ulinganishi viwango, maoni ya wadau, na maoni ya Kamati ya Ushauri kulinagana na mahitaji ya jamii.

Katika Programu zilizopitiwa, 38 zitaendeshwa kwa njia ya ana kwa ana, 51 zitaendeshwa kwa njia mseto; ana kwa ana na kwa njia ya mtandao na 7 zitaendeshwa kwa njia ya mtandao. Mradi pia umetoa mafunzo kwa wanataaluma kuhusiana na mbinu bunifu za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kama zilivyoelezwa katika Mwongozo ulioandaliwa wa Mbinu bunifu za Ufundishaji. Mwongozo wa mafunzo unatoa mwongozo wa namna mbinu bunifu zinaweza kuhusishwa katika mapitio ya mitaala. Mbinu bunifu na zana za kitehama vimezingatiwa katika makundi yote ya wajifunzaji ikiwa ni pamoja na wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Katika kipindi hiki, Chuo kimefanikiwa kutengeneza mfumo wa TEHAMA kwa ajili ya uendeshaji wa majarida ya UDSM na kutoa mafunzo kwa watawala, waratibu wa majarida, watoa mafunzo, na timu za kiufundi katika eneo la ubunifu na uatamizi. Chuo kimeandaa na kuufanyia majaribio mfumo wa kitehama wa uendeshaji wa majarida. Mafunzo kuhusiana na masuala ya ubunifu na uatamizi yanaendelea tukiwa tunaendelea na hatua za uchapishaji wa jarida letu.

Kamati za Ushauri zimeendesha mikutano yake kama ilivyopangwa na zimeendelea na jukumu la kujenga uhusiano baina ya mfumo wetu wa elimu na mahitaji ya jamii katika tasnia mbalimbali. Kufuatia jitihada katika utekelezaji wa Mradi, hadi sasa Chuo kimekwishasaini mikataba tisa ya maridhiano na makampuni mbalimbali kwa lengo la kuimarisha uhusiano baina ya Chuo na tasnia mbalimbali.

Uambatishaji wa wafanyakazi katika tasnia mbalimbali umepata umaarufu na kuwavutia wadau mbalimbali kutoka ndani na nje ya maeneo ya vipaumbele. Mpaka sasa wafanyakazi 27 wako katika programu ya uambatishaji inayotarajiwa kukamilika ifikapo Novemba 2024. Aidha, Chuo kimewapokea kwa furaha wanataaluma watatu baada ya kuhitimu masomo yao ya shahada ya umahiri nchini Uingereza na kufanya idadi ya wahitimu waliorejea kazini kufikia wanane.

Katika kipindi hiki pia kuna matukio mawili muhimu yamefanyika ambayo ni ubainishaji wa wadau wa mapambano ya ukatili wa kijinsia na uzinduzi wa mfumo wa ushughulikiaji wa malalamiko katika maeneo ya ujenzi. Aidha, kumetolelewa mafunzo kwa wadau wa mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia. Kufuatia uanzishwaji wa mfumo wa kushughulikia malalamiko, Chuo kimepokea malalamiko na mapendekezo kuhusiana na Mradi na kuishughulikia kwa njia ya mfumo.

Katika mchakato wa utekelezaji wa Mradi, Chuo kimebaini changamoto za kiutekelezaji kutokana na sababu mbalimbali kama kupanda kwa gharama za uendeshaji. Chuo pia kinatambua mahitaji mapya yaliyojitokeza ambayo yanahitajika kutiliwa maanani hususani katika ujenzi wa kampasi mpya. Wataalamu wetu wanaandaa mikakati ya namna ya kuzingatia mahitaji haya ikiwa ni pamoja kukamilisha Mpango Endelevu wa utelezaji wa mradi.

Maendeleo haya yamefanikiwa kutokana na ushirikiano na msaada tulioupata kutoka kwa wadau mbalimbali. Tunatoa wito kwa wadau wote kuendelea kukiunga mkono Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili kufanikisha utekelezaji wa miradi mbalimbli.

# UDSM chakabidhi maeneo ya HEET kwa wakandarasi kwa ajili ya Ujenzi

*Na Ally Mambele, UDSM-HEET*



Ujenzi ukiendelea katika maeneo yanapojengwa majengo ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kupitia mradi wa HEET Kagera, Lindi, Zanzibar na Dar es Salaam. Picha hizi zimepigwa hivi karibuni.






Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimekabidhi maeneo yake ya ujenzi wa majengo 24 chini ya Mradi wa HEET kwa wakandarasi wanaohusika, huku kukiwa na mustakabali wenye matarajio mengi, imeelezwa.

Kukabidhi maeneo haya, ambako kumekuwa hatua muhimu na maendeleo katika dhamira ya UDSM ya kuimarisha miundombinu ya elimu ya juu nchini Tanzania, kumethibitisha kuwapo kwa UDSM kwa wakazi wa mikoa ya Lindi na Kagera.

"Mradi huu wa HEET ambao unafadhiliwa na Benki ya Dunia, lengo lake ni kuimarisha uwezo wa taasisi za elimu ya juu kuchangia katika ukuaji na maendeleo ya uchumi wa taifa. Hivyo, tumekabidhi maeneo ya ujenzi kwa wakandarasi ambao wameahidi kukamilisha kazi hiyo," amesema Dkt. Liberato Haule, Naibu Mratibu wa HEET-UDSM.

Dkt. Haule aliongeza kuwa miongoni mwa maeneo yaliyokabidhiwa ni Jengo la Jinsia na watu wenye Mahitaji Maalum katika Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere Mlimani, Dar es Salaam, ambalo limetengewa nafasi maalum inayotoa huduma muhimu kama vile unasihi, upatikananji wa rasilimali, na programu maalum kwa makundi ya jinsia na wanafunzi wenye ulemavu.

"Kituo hiki, kina umuhimu mkubwa katika kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wanapata rasilimali na msaada unaohitajika ili kufanikiwa kitaaluma", amesema Dkt. Haule

Jengo lingine linalojengwa Dar es Salaam ni hosteli ya wanafunzi wa uzamili ambayo itahudumia mahitaji yanayokua ya malazi ya ubora wa kiwango cha juu ya kampasi kwa wanafunzi wa uzamili. Jengo hili likiwa na mandhari ya kisasa, litakuwa na mazingira mazuri ya kuishi ili kusaidia juhudi za kitaaluma za ngazi ya juu katika UDSM.

Wakati wa hafla ya kukabidhi, Dkt. Paul Ndumbaro, Mtaalamu wa Maendeleo ya Miundombinu wa UDSM-HEET, alisisitiza umuhimu wa majengo haya ambayo "yanawakilisha jitihada zetu zisizoyumba ya ujumuishaji, uanuwai, na ubora wa kitaaluma".

Alisema kuwa jengo la Jinsia na Mahitaji Maalum pamoja na Hosteli ya Uzamili ni maeneo muhimu ya mkakati wa kutengeneza mazingira ambayo kila mwanafunzi atafanikiwa.

Mwakilishi wa mmoja wa wakandarasi, Mohamed Builders Ltd., alikihakikishia Chuo Kikuu kuhusu kujizatiti kwao kukamilisha miradi kwa wakati, kuzingatia ubora, utumikaji, ufikikaji, na uendelevu. Ujenzi wa majengo yote unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 18.

### *Matokeo ya mradi wa HEET yadhihirika hadi nje ya Dar es Salaam*

Kwa kuendeleza maendeleo muhimu ya miundombinu huko Kagera, Lindi, na Zanzibar. Kwa mfano, eneo la Kagera litajikita katika kutoa elimu ya taaluma za kilimo na biashara. Mradi huu, wenye bajeti ya shilingi bilioni 13.17, unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 18.

Kwa upande wa Zanzibar, UDSM imekabidhi eneo la ujenzi katika Taasisi ya Sayansi za Bahari (IMS) kwa ajili ya ujenzi wa jengo jipya lililotengwa kwa ajili ya sayansi za bahari. Jengo hili litaboresha kwa kiasi kikubwa uwezo wa Taasisi ya Sayansi za Bahari katika kufanya utafiti wa ngazi za juu na kutoa mafunzo maalum katika taaluma za bahari na pwani na kuchangia katika uendelevu wa kiuchumi na mazingira wa Zanzibar.

Dkt. Ndumbaro alisisitiza umuhimu wa kimkakati wa jengo hili kwa Zanzibar, akisema kuwa litakuwa uwekezaji mkubwa katika siku zijazo za sayansi za bahari

*Inaendelea uk. 15...*

# Bunge lakipongeza Chuo katika Utekelezaji wa Mradi wa HEET

*Na Jackson Isdory na Tumaini Kibangala, UDSM-HEET*



*Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo wakiongozwa na Mwenyekiti wa Kamati, Mhe. Husna Juma Sekiboko (Mb.) (wa nne kushoto) na baadhi ya viongozi na wafanyakazi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wakiongozwa na Mwenyekiti wa Baraza la Chuo, Mhe. Balozi Mwanaidi Maajar (wa tatu kushoto) na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo-Mipango, Fedha na Utawala (wa pili kushoto) wakati Kamati ilipotembelea Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili kufahamu kuhusu utekelezaji wa Mradi wa HEET, hivi karibuni.*

Kamati ya Kudumu ya Bunge inayosimamia masuala ya Elimu, Utamaduni na Michezo imekipongeza Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika jitihada zake za dhati za kuboresha elimu nchini kupitia Mradi wa HEET.

Pongezi hizi zilitolewa wakati wa ziara ya Kamati kwa lengo la kukagua utekelezaji wa shughuli mbalimbali zinazofanyika chini ya Mradi wa HEET. Kamati ilifanya ziara katika Taasisi ya Sayansi za Bahari (IMS) huko Zanzibar tarehe 9 Septemba 2024 na baadaye tarehe 10 Septemba 2024 Kamati ilifanya ziara yake katika Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere Mlimani.

Wajumbe wa Kamati hii wakiongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Husna Sekiboko (Mb.) walioneshwa kuridhishwa kwao na hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Mradi wa HEET kwa kueleza kwamba UDSM kimepiga hatua kubwa katika maeneo mbalimbali ya utekelezaji wa Mradi. Maeneo hayo ni pamoja na ujenzi wa miundombinu na mapitio ya mitaala ili kuhakikisha kwamba mitaala yake inaendana na mahitaji ya jamii kitaifa na kimataifa.

"Mapitio ya mitaala yatasaidia katika kukabiliana changamoto za kukosekana kwa fursa za ajira nchini Tanzania kwa kuwa mapitio haya mbali na mambo mengine yanahakikisha kwamba elimu inayotolewa inawaandaa wahitimu kutumia maarifa waliyoyapata ili kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili jamii ikiwa ni sehemu mojawapo ya fursa ya ajira", amesema Mhe. Sekiboko.

Ameongeza kwamba "Kuna umuhimu wa kujitathmini ili kujiridhisha kwamba elimu tunayoitoa inatusaidia katika kukabiliana na changamoto zinazotusibu. Ni muhimu tukajiuliza, Je, wahitimu wetu wana uwezo wa kutatua matatizo yanaikabili jamii?"

Mhe. Sekiboko alikipongeza Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kueleza kwamba Kamati imefurahishwa na jitihada za Chuo katika utekelezaji wa malengo ya Mradi wa HEET. Aidha, amewataka wahusika wote wakiwamo wakandarasi kuhakikisha kwamba wanakamilisha shughuli zao kwa wakati.

*Inaendelea uk. 7...*



# Bunge lakipongeza Chuo....

*(Inatoka uk. 6)*

## UDSM kuchangia katika maendeleo ya Taifa

Katika ziara hii wajumbe waliambatana na Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Omary Kipanga (Mb.) pamoja Katibu Mkuu wa Wizara Prof. Carolyne Nombo.

Kamati ilikagua shughuli mbalimbali zinazotekelezwa chini ya Mradi wa HEET ikiwa ni pamoja na ujenzi wa bweni litakalokuwa na uwezo wa kuchukua wanachuo 40 huko IMS, Zanzibar, madarasa 4 yatakayokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 216, ukumbi wa mikutano wenye uwezo wa kuchukua watu 150, ofisi za wafanyakazi, na maabara 5

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Omary Kipanga alisisitiza kwamba wizara anayoiongoza itaendelea kusimamia kwa karibu utekelezaji wa Mradi wa HEET pamoja na miradi mingine ya maendeleo inayotekelezwa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili kuhakikisha kwamba UDSM kinaendelea kuchangia katika maendeleo ya taifa.

"Hiki ni Chuo chetu na ni lazima kifuate maelekezo ya Kamati ya Bunge na miongozo ya Serikali ili kufikia malengo ya taifa. Tunapaswa kuhakikisha kwamba tunafundisha, tunafanya utafiti na kutoa huduma kwa jamii hivyo kuchangia moja kwa moja katika maendeleo ya taifa. Ninampongeza Rais wa Jamahuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jitihada anazozifanya kuboresha sekta ya elimu nchini Tanzania", amesema Mhe. Kipanga

Kwa upande wake Makamu Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Mussa Sima (Mb.) alisisitiza kwamba Chuo kinapaswa kuhakikisha kwamba matokeo ya utafiti unaofanywa na wanataaluma yanatolewa kwa lugha inayoweka kwa urahisi kwa wananchi.

"Vyuo vyetu vikuu ikiwa ni pamoja na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam vinafanya tafiti nyingi. Matokeo ya tafiti hizi hayana budi kufahamika katika jamii ili waweze kuyaona na kutambua mchango wetu katika kutatua changamoto zao. Hili linawezekana ikiwa tutatumia lugha inayofahamika na jamii inayotuzunguka badala ya kufanya tafiti na kisha kuhifadhi matokeo ya tafiti hizo katika mashubaka", amesema Mhe. Sima.



*Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Mhe. Balozi Mwanaidi Maajar (katikati) akizungumza na baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo.*

## Mradi wa HEET kuacha alama ya kukumbukwa

Kwa upande wake Naibu Makamu Mkuu wa Chuo, Mipango, Fedha na Utawala Prof. Bernadeta Killian, ambaye pia ni Mratibu wa Mradi wa HEET aliihakikishia Kamati ya Bunge kwamba Chuo kitafanya kila linalowezekana kuhakikisha kwamba Mradi wa HEET unatekelezwa na kuwezeshwa kwa wakati na kwa kiwango kilichokusudiwa.

"Tutahakikisha kwamba Mradi wa HEET siyo tu kwamba unakamilika kwa ufanisi bali utaacha alama ya kukumbukwa kwa Chuo na kwa Taifa kwa ujumla. Tutahakikisha kwamba tunatumia fedha kwa malengo yaliyokusudiwa, tutaboresha mitaala yetu ili kuwawezesha wahitimu wetu wanapata elimu inayoendana na mahitaji ya soko na kwamba jamii inanufaika na matokeo ya Mradi huu", amesisitiza Prof. Killian.

Ameongeza kwamba utekelezaji wa shughuli za ujenzi chini ya Mradi wa HEET unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 18 na utagharimu TZS11,194,677,531.

Mwenyekiti wa Baraza la Chuo, Mhe. Balozi Mwanaidi Maajar aliwashukuru wajumbe wa Kamati ya Bunge kwa ziara waliyoifanya pamoja na maelekezo na ushauri walioutoa na kusisitiza kwamba Baraza litaendelea kufuatilia kwa karibu kuhakikisha kwamba Chuo kinayafikia malengo yaliyokusudiwa.

"Mheshimiwa Mwenyekiti na wajumbe wote, asanteni sana kwa ziara yenu na ninakuahidini kwamba Baraza litahakikisha kwamba Chuo kinaweka mikakati thabiti kuhakikisha kwamba kinatekeleza Dira ya UDSM ya 2061 na malengo ya taifa kwa ujumla", alihitimisha Balozi Maajar.





**Juu:** *Prof. Nelson Boniface, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo-Utafiti (kushoto) na Dkt. Peter Kisenge, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) wakibadilishana nyaraka zinavyohusu ushirikiano baina ya taasisi hizi mbili.*

**Kulia:** *Baadhi ya Viongozi na Wafanyakazi wa UDSM na JKCI wakiwa kwenye kikao kujadili masuala mbalimbali kuhusu ushirikiao baina ya taasisi hizo.*



# Mpango wa pili wa uambatishaji wa wafanyakazi wazinduliwa kwa ari kubwa

Na Jackson Isdory, HEET-UDSM

Katika mkakati wa kuendelea kujenga uhusiano madhubuti baina ya ujuzi wa kitaalamu na uwanja taaluma, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimezindua mpango wa pili wa uambatishaji wa wafanyakazi kwa mwaka wa masomo 2023/2024.

Programu hii itakayoendeshwa baina ya Septemba na Disemba 15 itashuhudia jumla ya wafanyakazi 27 wakipata ujuzi na uzoefu katika tasnia mbalimbali nchini Tanzania. Programu hii mbali na mambo mengine inalenga kukuza ujuzi na kuimarisha ushirikiano baina ya maarifa ya kitaaluma na utendaji halisi katika tasnia mbalimbali.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Prof. William A. L. Anangisye alitoa shukrani zake za dhati kwa asasi zilizowapokea wafanyakazi hao na kusisitiza wajibu wao kama wadau muhimu katika dhamira ya UDSM kuboresha ubora wa elimu inayotolewa chuoni na hatimaye kuwa na mitaala inayoendana na mahitaji halisi ya jamii.

“Tunazishukuru kwa dhati asasi zilizokubali kuwapokea wafanyakazi wetu katika mpango wa uambatishaji wa wafanyakazi. Ubia huu ni zaidi ya ushirikiano baina ya UDSM na tasnia mbalimbali; ni njia mojawapo ya kujenga mfumo wa kiikolojia katika ufundishaji na ujifunzaji ambao utasaidia kushughulikia masula muhimu ya kitaifa hususani suala la ajira kwa vijana kama ambavyo imekuwa ikielekezwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan”, amesema Prof. Anangisye

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo-Utafiti, Prof. Nelson Boniface kwa upande wake ameonesha matumaini yake kuhusu manufaa ya mpango huu. “Tunaamini kwamba programu hii itatoa fursa muhimu katika kukuza ujuzi na kupiga hatua. Tunatarajia mpango huu utawanufaisha washiriki, UDSM na taifa kwa ujumla”.

Dkt. Eva Shayo ambaye ni Mratibu wa Ushirikiano baina ya Chuo na tasnia mbalimbali, amebainisha umuhimu wa programu hii wafanyakazi na Chuo na namna ambavyo uteuzi wa wafanyakazi hawa ulivyozingatia suala la mtawanyo na ujumuishwaji.

“Lengo letu ni kuwa na kundi linalohusisha washiriki kutoka katika vitengo mbalimbali ndani ya UDSM kwa lengo la kukuza ujuzi na uzoefu. Tunashukuru kwa ushirikiano huu madhubuti baina ya Chuo na tasnia mbalimbali zilizowezesha kupatikana kwa fursa ya kuchukua kundi hili la wafanyakazi”, Dkt. Shayo alifafanua

Dkt. Shayo alieleza kwamba programu hii iliwavutia wafanyakazi wengi ambapo jumla ya wafanyakazi 38 kutoka katika vitengo mbalimbali vya kitaaluma na kiuendeshaji waliomba fursa hii.

“Ili kuhakikisha kwamba haki inatendeka na uwazi unazingatiwa katika mchakato wa kuwapata wahusika, Kamati maalumu iliteuliwa ili kupitia maombi ya kila mmoja kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa. Mchakato wa uteuzi ulizingatia vigezo mbalimbali kama vile uzoefu, fursa ya ukuaji, na kuendana na malengo ya program”, alisema.

Dkt. Shayo alifafanua kuwa ili kuwa na programu yenye manufaa, vigezo mbalimbali viliwekwa kwa waombaji na asasi wanazotaka kwenda. “Mwombaji anapaswa kuwa mwajiriwa wa UDSM siyo chini ya miaka mitatu kabla ya umri wa kustaafu, asiwe likizo na awe na awe tayari kuzingatia vigezo na masharti ya asasi mwenyeji”.

Alieleza kwamba asasi mwenyeji kwa upande wake inapaswa kujiimarisha kiteknolojia, kuwa mashuhuri na kuendana na ujuzi wa mwombaji.

*inaendelea uk. 15...*

# Kamati ya MELL yajizatiti kama nguzo muhimu kwa mafanikio ya utekelezaji wa HEET

*Na Remmy Wilson, UDSM-HEET*



*Kamati ya Ufuatiliaji, Tathmini na Mafunzo (MELL) katika Mradi wa HEET Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ikiongozwa na Mweyekiti wake Dkt. Innocent Pantaleo, ikiwa katika moja ya vikao vyake.*

Wakati Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kikiweka jitihada kubwa katika utekelezaji wa Mradi wa HEET, Kamati ya Ufuatiliaji, Tathmini na Mafunzo (MELL) imeeleza majukumu yake muhimu katika kuhakikisha ubora na ufuatiliaji wa utekelezaji huo.

Akizungumza na Jarida hili hivi karibuni, Dkt. Innocent Pantaleo, Mwenyekiti wa Kamati ya MELL na Mtaalamu wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mradi wa HEET-UDSM, alisema kwamba Kamati hii ina jukumu la kufuatilia maendeleo, kuhakikisha kufuatwa kwa mipango, na kutoa ripoti, imekuwa na mchango mkubwa katika mafanikio ya mradi wa HEET-UDSM.

"Kamati ya MELL imekuwa na jukumu kubwa la kufuatilia Mradi wa UDSM-HEET kwa kutumia mbinu kuu mbili: ufuatiliaji wa ana kwa ana na ufuatiliaji wa viashiria. Ufuatiliaji wa ana kwa ana unajumuisha ziara za maeneo yanayohusika ili kuhakikisha kwamba ujenzi na miradi mingine vinafuata viwango vilivyoainishwa katika Mpango Mkakati wa Uwekezaji wa Chuo (USIP) na Mpango wa Matokeo ya Maendeleo ya Mradi (PDO)", amesema Dkt. Pantaleo.

Kuhusu suala la ufuatiliaji wa viashiria, Dkt. Pantaleo aliongeza, "kamati inafuatilia maendeleo ya mradi kupitia ripoti za wataalamu, zikijumuisha kila kitu kuanzia mchakato wa ununuzi hadi mafunzo ya uanagenzi kwa wanafunzi na upatikanaji wa ithibati ya mitaala."

Dkt. Pantaleo alisisitiza kwamba matokeo hayo yanajumuishwa katika ripoti za kila mwezi na kila robo mwaka, ambazo huwasilishwa katika Kitengo cha Utekelezaji wa Mradi (PIU), Kamati ya Uendeshaji, na kuwasilishwa kwa Wizara. "Kuhusu kutathmini maendeleo, kamati ya MELL inazingatia matumizi mbinu faafu. Tunagawa kila shughuli katika shughuli ndogo, kila moja ikiwa na tarehe ya mwisho ya utekelezaji. Mgawanyo huu madhubuti unaruhusu kamati kutathmini ikiwa wataalamu wa mradi wanafanikisha malengo yao na, kama sivyo, kamati inashughulikia changamoto au ucheleweshaji wowote," ameongeza.

Dkt. Pantaleo alielezea kwamba kamati inatumia bangokitita la matokeo kufuatilia maendeleo kulingana na viashiria vitatu vikuu vya Ofisi ya Utekelezaji wa Mradi, walengwa wa mradi, uhusiano wa kitasnia (ajira za wafanyakazi na wanagenzi katika tasnia), na uthibitishaji wa mitaala (kuhakikisha kwamba mitaala iliyorekebishwa inakidhi viwango vya kimataifa).

"Kamati inafuatilia viashiria vya kati, ambavyo vinajumuisha usawa wa kijinsia, ushughulikiaji wa malalamiko, kozi za mabadiliko ya tabianchi, na maendeleo ya ujenzi, ili kuhakikisha utendaji mzuri wa mradi na kuendana na malengo makuu. Tumefanikiwa kufuatilia maendeleo ya mradi, bila matatizo makubwa au viashiria vyovyote vya hali hatarishi. Mradi uko kwenye njia sahihi," alisema kwa kujiamini.

Ili kuhakikisha ufanisi na umadhubuti wa MELL na Mradi wa HEET, Dkt. Pantaleo alisisitiza pia umuhimu wa kutumia Mfumo Jumuishi wa Usimamizi (IMS) katika kuripoti kuhusu Mradi. "Mfumo huu unafanya kazi na unarahisisha ufuatiliaji wa shughuli kuu na shughuli ndogo. Tunawahimiza wataalamu wote kuutumia".

## Muundo wa MELL

Dkt. Pantaleo alielezea kwamba MELL inaundwa na wanachama wanne wa kudumu, kila mmoja akileta utaalamu wa kipekee, unaoakisi mahitaji mbalimbali ya Mradi wa

*inaendelea uk. 17...*

# Ujumbe wa Naibu Mratibu



## Dr. Liberato Haule

**Naibu Mratibu HEET - UDSM**

Kitengo cha Utekelezaji wa Mradi kinafurahi kuwajulisha wasomaji wake kuhusu hatua mbalimbali zilizofikiwa katika utekelezaji wa Mradi wa HEET kuanzia tulipotoa taarifa katika toleo la tano.

Kufutia kusainiwa kwa mikataba ya shughuli za ujenzi mwezi Februari na Mei 2024, shughuli halisi za ujenzi zimeanza mwezi Aprili na Julai 2024 mtawalia. Kwa mujibu wa mikataba iliyosainiwa, shughuli za ujenzi zinapaswa kukamilika kabla au ifikapo mwezi Novemba 2025.

Baada ya kukamilika kwa shughuli hizi za ujenzi, UDSM kitakuwa na jumla ya ofisi 52, maabara 7 karakana 5, na ukarabati wa majengo katika bloku L, O na Q yaliyopo katika ndaki ya Uhandisi na Teknolojia. Ujenzi wa majengo mapya katika Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia utasaidia kupatikana kwa nafasi kuwahudumia wanafunzi kwa idadi inayoonekana kwenye mabano. Ukumbi wa mhadhara (250), vyumba vya madarasa (84), karakana (150), maabara (420), chumba cha studio kwa ajili ya programu ya usanifu vitambaa (45) na hosteli (50). Aidha, kutakuwa na Jengo la Jinsia na watu wenye mahitaji maalum katika Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere Mlimani.

Ujenzi wa jengo la TEHAMA katika Ndaki ya Habari na Mawasiliano iliyopo Kijitonyama, Dar es Salaam utawezesha kupatikana kwa nafasi za wanafunzi kwa idadi kama inavyoonekana katika mabano; ukumbi wa mhadhara (140), karakana (60), maabara (96), na studio (50). Aidha, Jengo jipya katika Shule Kuu ya Sayansi Akua na Uvuvi huko Kunduchi, Dar es Salaam utasaidia kupatikana nafasi kwa idadi kama inavyoonekana katika mabano; ukumbi wa muhadhara (300) na Maabara (50).

Upanuzi katika Taasisi ya Sayansi za Bahari huko Buyu, Zanzibar utasaidia kupatikana kumbi zitakazowezesha kuwahudumia wanafunzi kwa idadi kama inavyoonekana katika mabano; kumbi za mihadhara (216), maabara (125), ukumbi wa mikutano (150), na hosteli (40). Aidha, utawezesha kupatikana kwa ofisi mbalimbali za wafanyakazi.

Kampasi mpya katika Mkoa wa Kagera itawezesha kupatikana kwa nafasi mpya kwa idadi kama inayoonekana katika mabano; kumbi za mihadhara (440), vyumba vya madarasa (280), maabara (70), kafeteria (70) na hosteli (70).

Kukamilika kwa majengo haya kwa wakati kutafanikisha utekelezaji wa mitaala iliyoboreshwa ambayo iko katika hatua za mwisho za kupata ithibati. Uboresha wa miundombinu ya TEHAMA utaleta mapinduzi makubwa katika mfumo wa ufundishaji na utafiti.

Kitengo cha Utekelezaji wa Mradi kimeanza mchakato wa ununuzi wa vifaa vya vya ufunzaji na ujifunzaji ambavyo vitawekwa katika majengo mapya yanayojengwa. Wataalamu wamekwishabainisha vifaa vinavyohitajika kwa kuzingatia mahitaji ya mitaala iliyoboreshwa na rasilimali zilizopo.

Tunawatakia wasomaji wetu usomaji mwema wa toleo hili. Aidha, Kitengo cha Utekelezaji wa Mradi, kinatambua jitihada za mtu mmoja mmoja na taasisi mbalimbali ambazo zimechangia kupatikana kwa manufaa yaliyoainishwa katika toleo hili.

# Tahariri

## Kongole Maendeleo ya ujenzi katika Mradi wa HEET UDSM

Imeripotiwa katika jarida hili kwamba maendeleo ya ujenzi katika majengo 24 yanayojengwa chini ya Mradi wa HEET UDSM katika mikoa ya Dar es Salaam, Zanzibar, Lindi (Ngongo na Ruangwa) na Kagera ni ya kuridhisha; hali inayoashiria kukamilika kwa wakati kwa miradi hii kama ilivyosainiwa katika mikataba.

Maendeleo haya yamefikiwa miezi michache baada ya kusainiwa kwa mikataba ya ujenzi mwezi Februari na Mei 2024 ambapo ujenzi halisi ulianza mwezi Aprili na Julai 2024 mtawalia.

Kwa hakika hizi ni habari njema na zinazostahili pongezi kwa kuzingatia kwamba Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimedhamiria kuhakikisha kwamba ujenzi wa majengo haya unakamilika kabla au ifikapo Novemba 2025.

Suala la mazingatio ya muda kutoka kwa wakandarasi na wadau wengine wanaohusika linatia matumaini jambo ambalo linaoonesha umuhimu wa kuendelea kushirikiana ili kuhakikisha kwamba chagamoto yoyote itakayojitokeza inakabiliwa kwa wakati ili kutokukwamisha shughuli za utekelezaji wa Mradi.

Kama ambavyo imekuwa ikiripotiwa mara kwa mara, shughuli za ujenzi katika Mradi wa HEET UDSM zimechukua sehemu kubwa ya fedha za Mradi, kufikia USD milioni 31.9 (takribani asimilia 67.3) katika fedha zilizotolewa kwa UDSM ambazo ni USD milioni 47.5.

Mradi huu utakapokamilika utakipatia UDSM majengo mapya na kufanikisha ukarabati wa majengo yaliyokuwepo na hivyo kusaidia katika kupatikana kwa ofisi, karakana, kumbi za mihadhara, maabara, hosteli na jengo la masuala ya jinsia na watu wenye mahitaji maalum.

Mchango mwingine mkubwa wa Mradi huu ni ujenzi wa Kampasi mbili mpya katika mikoa ya Kagera na Lindi ambapo fani za biashara na kilimo mtawalia zitatolewa katika kampasi hizo.

Kwa kuzingatia maendeleo yaliyofikiwa hadi sasa ambapo tumeelezwa kwamba wakandarasi wako ukingoni kukamilisha hatua ya awali ili waendelee na hatua inayofuata, tunapongeza jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na Chuo Kikuu cha Dar es salaam pamoja na wadau wengine wanaohusika katika mradi huu kwa namna moja au nyingine.

Tunatoa wito kwa wahusika wote kuendeleza jitihada hizi ili kuleta ufanisi katika utelezaji wa Mradi kwa wakati kama ilivyofanyika katika awamu hii ambayo iko ukingoni kumalizika.


### Uratibu wa Mradi wa HEET-UDSM

**Mratibu wa Mradi**
Prof. Bernadeta Killian

**Naibu Mratibu wa Mradi**
Dkt. Liberato V. Haule

### Timu ya Uhariri


**Mhariri Mkuu &**
**Mtaalamu wa Uhusiano kwa Umma na Mawasiliano HEET-UDSM**
Dkt. Dotto Paul Kuhenga

**Waharir**i
Dkt. Lupa Ramadhani (Kiingereza)
Dkt. Mussa Hans (Kiswahili)

**Waandishi:**
Jackson Isdory
Zamda George
Ally Mambele
Mercy Machange
Remmy Wilson

**Mpiga Picha:**
Tumaini Kibangala

**Msanifu**
Michael Mwakatobe

# Matukio katika Picha





**Maazimio:** Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo wakiongozwa na baadhi ya viongozi na wafanyakazi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wakati Kamati ilipotembelea Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili kuona utekelezaji wa Mradi wa HEET, hivi karibuni.








**Mipango kwa ajili ya Matokeo Makubwa:** Kikao cha 7 cha Kamati ya Taasisi ya Usimamizi ya Mradi wa HEET Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilichofanyika tarehe 21 Agosti, 2024, Kibaha, Pwani.





**Matarajio Chanya:** Waandishi wa Habari na baadhi ya Wataalamu wa Kamati ya Utekelezaji wa Mradi wa HEET Chuo Kikuu cha Dar es Salaam walipotembelea eneo ambapo ujenzi wa majengo ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kupitia mradi wa HEET, katika Mkoa wa Lindi unaendelea.







**Ushirikishwaji na Usalama:** Ubainishaji na Mafunzo kuhusu Ukatili wa Kijinsia kwa watoa huduma katika maeneo mbalimbali ya ujenzi wa Mradi wa HEET UDSM nchini Tanzania chini ya Mratibu wa masuala ya Jinsia wa Mradi wa HEET-UDSM na Mkurugenzi wa Taasisi ya Jinsia, Dkt. Lulu Mahai (katikati-aliyesimama).

# Ujenzi wa Majengo HEET - UDSM

**Ujenzi wa majengo ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kupitia mradi wa HEET ukiendelea katika maeneo ya Kagera, Lindi, Zanzibar na Dar es Salaam.**

















# Mapitio ya Mitaala UDSM yafanyika kwa mafanikio

*Na Zamda George, HEET- UDSM*



*Washiriki wa warsha ya siku mbili kuhusu mchakato wa mapitio ya mitaala katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam iliyofanyika Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere Mlimani hivi karibuni. Warsha hii ilihudhuhuriwa na washiriki zaidi ya 150 ikiwemo viongozi wakuu wa chuo, marasi, maamidi na wakurugenzi, wakuu wa idara, waratibu wa mitaala na wapitiaji wa mitaala kutoka katika vitengo mbalimbali vya kitaaluma.*

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimepiga hatua kubwa katika mpango wake wa kupitia na kuiboresha mitaala 98 ya shahada za awali na uzamili kufikia Julai 2024, Jarida hili limebaini.

Prof. Masoud Muruke, Mratibu wa Upitiaji wa Mitaala katika Mradi wa HEET UDSM ameeleza kwamba mafanikio ya mchakato wa upitiaji wa mitaala yanatokana na mpango thabiti wa Chuo kuboresha programu zake na hatimaye kuzalisha wahitimu watakaozingatia mahitaji ya sasa ya soko la ajira.

"Mchakato wa mapitio ya mitaala siyo tu kwamba unahusisha uboreshaji wa kozi mbalimbali bali pia unaangazia mbinu bunifu zitakazozalisha wanafunzi watakaoendana na mabadiliko yanayotokea katika jamii. Tunahakikisha kwamba wahitimu wetu wana ujuzi na maarifa yatakayowawezesha kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili jamii", amesema Prof. Muruke.

Prof. Muruke amesema pia kwamba mapitio ya mitaala yamezingatia matumizi ya mbinu mseto kwa programu 38 za shahada za awali na 28 za shahada za uzamili. Uanzishwaji wa programu zitakazoendeshwa kwa njia ya mtandao umepanua wigo wa kupata elimu ya juu kwa wadau mbalimbali na kuifanya UDSM kuendelea kuwa kinara katika matumizi ya mbinu bunifu katika mfumo wa elimu.

"Tunaanzisha mbinu mpya za ufundishaji kwa lengo la kuwa na mazingira jumuishi ya ujifunzaji, ambapo wanafunzi wanaweza kunufaika kwa mbinu zilizozoeleka na mbinu za dijitali katika ufundishaji", ameongezea Prof. Muruke.

Prof. Muruke ameeleza kwamba warsha ya siku mbili inayohusu mchakato wa mapitio ya mitaala iliyofanyika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kuwashirikisha washiriki zaidi ya 150 ikiwa ni pamoja na wajumbe wa menejimenti, marasi, maamidi na wakurugenzi, wakuu wa idara, wakuza mitaala imelenga kuwaweka pamoja wadau hawa kwa lengo la kujadili namna ya kuboresha mitaala ya UDSM.

"Warsha hii iliwapa fursa washiriki kupata mrejesho, kuzingatia mafunzo yanayotokana na ziara ya ulinganishi viwango iliyoangazia maeneo mbalimbali kama usawa wa kijinsia na uendelevu wake pamoja na ushirikiano baina ya UDSM na wadau wengine. Hii ni fursa kwetu kuboresha mustakabali wa programu zetu", amesema Prof. Muruke.

Aidha, katika warsha hii washiriki walijadili namna ya kuzingatia mbinu za kiteknolojia katika mitaala, hatua itakayoifanya elimu inayotolewa UDSM kuzingatia mfumo wa dijitali wa unaotumiwana vyuo vingine ulimwenguni. Hatua inayofuata ni kukamilisha mchakato wa mapitio ya mitaala ili kuiwasilisha Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania.

Prof. Bonaventure Rutinwa, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo - Taaluma amesisitiza umuhimu wa kukamilisha mchakato wa mapitio kwa haraka na kwa viwango vinavyotakiwa kwa kuzingatia kwamba haya ni mapitio ya kimkakati kuhakikisha kwamba programu zote zinaendana na viwango vya kidunia kama vile mageuzi ya dijitali, uendelevu na elimu ya fedha.

Prof. Bonaventure Rutinwa, ameendelea kueleza kwamba lengo la mchakato huu ni kuhakikisha kwamba UDSM inaendelea kuwa kinara katika utoaji wa elimu ya juu kikanda na kidunia.

"Tumedhamiria kuzalisha wahitimu ambao siyo tu kwamba watakuwa na uwezo wa kitaaluma bali pia uwezo wa kuleta mabadiliko katika jamii zinazowazunguka", amesema Prof. Rutinwa.

Mapitio ya mitaala yalianza kwa kufanya tathmini ya programu zinazofundishwa, kazi ambayo ilifanywa na wataalamu wa ndani na nje na wadau kutoka tasnia mbalimbali ambao waliainisha maeneo yanayohitaji kuboreshwa.

Mchakato huu pia ulihusisha ziara ya ulinganishai viwango iliyofanyika katika vyuo vikuu vyenye hadhi ya juu nchini Afrika kusini, Ghana, Korea ya Kusini, na Ujerumani. Ziara hii imekuwa na manufaa makubwa katika mchakato wa mapitio ya mitaala na usimamizi wa utekelezaji wake.

## UDSM chakabidhi maeneo ya HEET ....

*(Inatoka uk. 5)*

nchini Tanzania. Litawapatia watafiti na wanafunzi wetu vifaa vya kisasa vya kuchunguza na kutatua changamoto zinazokabili mazingira yetu ya bahari.

Pia, katika Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere Mlimani, kuna matarajio ya kuboresha miundombinu muhimu katika Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia ambapo kuna ujenzi wa chumba cha studio kwa ajili ya programu ya usanifu vitambaa, Jengo la Karakana, na Jengo la Maabara, pamoja na ukarabati wa majengo katika bloku Q, O, na L.

"Maboresho haya yataboresha kwa kiasi kikubwa uwezo wa kampasi kusaidia mafunzo maalum na utafiti, hususani katika uhandisi vitambaa na teknolojia", amesema Dkt. Ndumbaro.

Wakati wa hafla ya kukabidhi, Mhandisi Isaya Anase wa UDSM alionesha kufurahia matokeo ya mradi huu, akisema, "Maendeleo haya si tu uwekezaji katika miundombinu yetu bali pia ni uwekezaji katika siku zijazo za elimu ya juu nchini Tanzania. Vifaa vipya vitawapa wanafunzi na watafiti wetu mazingira ya kiwango cha kimataifa ili wafanikiwe na kuwa wabunifu."

Mradi wa HEET, unaotokana na msaada kutoka serikali ya Tanzania na Benki ya Dunia, ni msingi wa mkakati wa UDSM wa kuhusianisha elimu ya juu na malengo ya taifa ya mabadiliko ya kiuchumi. Miradi ya ujenzi na ukarabati inayoendelea inatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 18, baada ya hapo itaanza kufanya kazi kikamilifu.

Maendeleo haya yanadhihirisha kujizatiti kwa UDSM katika kutoa elimu na fursa za utafiti, kukuza mazingira jumuishi ya kitaaluma, na kuchochea mabadiliko ya kiuchumi ya Tanzania kupitia elimu ya juu.



*Ujenzi wa majengo ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kupitia mradi wa HEET ukiendelea katika Taasisi ya Sayansi za Bahari (IMS), eneo la Buyu, Zanzibar.*

## Mpango wa pili wa uambatishaji...

*(Inatoka uk. 8)*

**Suala la mtawanyo lazingatiwa**

Dkt. Shayo alieleza kwamba mgawanyo wa wafanyakazi wanaume ambao 70.37% na wanawake ambao ni 29.63% katika taasisi binafsi ambazo ni sawa na 59.26% na taasisi za serikali ambazo ni sawa na 29.63% unadhihirisha namna ambavyo suala la mtawanyo limezingatiwa katika ukuzaji wa ubia baina ya Chuo na tasnia mbalimbali.

"Waombaji walioteuliwa watatawanywa katika asasi mbalimbali za kiserikali na zisizo za kiserikali. Mtawanyo huu umefanywa ili kuhakikisha kwamba wafanyakazi hawa wanapata ujuzi wa kiutendaji katika maeneo yao ya ubobezi", alisema Dkt. Shayo.

Akieleza kufurahishwa kwake kwa fursa hii mmoja wa wafanyakazi aliyeteuliwa katika Programu hii Arch. Mariam Marco Madundo ambaye ni Mhadhiri Msaidizi katika Idara ya Uhandisi Mihimili na Ujenzi, Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia anasema kwamba Programu hii ni zaidi ya fursa.

"Ni safari ya kuhusisha elimu yetu na ujuzi wa kitaalamu. Tunatamani kurudi na ujuzi wa kiutendaji ambao utatusaidia katika mbinu zetu za ufundishaji na hivyo kuwanufanisha wanafunzi wetu na Chuo kwa ujumla", amesema Arch. Madundo.



*Baadhi ya Viongozi na Wafanyakazi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) wakiwa kwenye kikao kujadili masuala mbalimbali kuhusu ushirikiao baina ya taasisi hizo.*



# Mapitio ya mitaala yazingatia mbinu bunifu na mafunzo ya ziara ya ulinganishi viwango

Na Zamda George, HEET- UDSM



**Mafunzo ya ziara ya ulinganishi viwango katika Chuo Kikuu cha Rhodes, Afrika Kusini:** *kutoka kushoto ni Dkt. Egbert Mujuni, Dkt. Aurelia Mallya, Prof. Nelson Boniface (Naibu Makamu Mkuu wa Chuo-Utafiti, UDSM), Dkt. Nomakwezi Mzilikazi, Dkt. Veronika Buchumi na Prof. Sizwe Mabizela (Makamu Mkuu wa Chuo-Rhodes).*

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimeendesha warsha kwa lengo la kujadili namna ya kuhusisha kipengele cha mbinu bunifu na mafunzo yaliyopatikana wakati wa ziara ya ulinganishi viwango katika maeneo mbali ulimwenguni. Uboreshaji huo umeifanya mitaala ya Chuo kuwa katika kiwango cha kimataifa.

Warsha hiyo iliyobeba mada kuu mbili ambazo ni mbinu bunifu na ripoti ya ziara ya ulinganishi viwango iliwakutanisha wadau kutoka katika vitengo mbalimbali. Washiriki walipokea ripoti ya ziara ya ulinganishi viwango iliyofanyika Afrika Kusini, Ghana, Korea Kusini na Ujerumani ambayo ilionekana kuwa na manufaa makubwa katika mitaala ya chuo ambayo iko katika mchakato wa kuboreshwa.

Washiriki wengine katika warsha hiyo walikuwa ni viongozi wakuu wa chuo, marasi, maamidi na wakurugenzi, wakuu wa idara, waratibu wa mitaala na wapitiaji wa mitaala kutoka katika vitengo mbalimbali vya kitaaluma.

Prof. Bonaventure Rutinwa, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma alisisitiza umuhimu wa mapitio ya mitaala kuzingatia mambo mazuri tuliyojifunza kutoka kwa wenzetu kwa mustakabali wa elimu tunayoitoa katika chuo chetu.

Alisisitiza dhamira ya Chuo katika kuzifanya programu zake kuwa katika kiwango cha kimataifa ili kuzalisha wahitimu watakaokuwa wameandaliwa vema katika kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazoisibu jamii.

"Kwa kawaida uboreshaji wa mitalaa ni mchakato endelevu unaohakikisha kwamba tunakwenda sambamba na mahitaji ya jamii kila uchao", amesema Prof. Rutinwa.

Zaidi ya washiriki 150 ambao ni wataalamu wa masuala ya elimu, watawala, wakuza mitaala, walishiriki katika warsha hiyo. Mchakato huu ulidhihirisha nia ya dhati ya Chuo kuhakikisha kwamba mitaala yake inaandaliwa kwa ubora wa hali ya juu kwa kuzingatia uzoefu kutoka katika vyuo vingine.

Katika warsha hii kulikuwa na mawasilisho mbalimbali ambapo viongozi wa misafara walipata fursa ya kubainisha mambo muhimu waliyojifunza wakati wa ziara ya ulinganishi viwango. Prof. Bernadeta Killian, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Mipango, Fedha na Utawala, aliwasilisha kuhusu mambo tunayoweza kujifunza kutoka Chuo Kikuu cha Memphis kwa kuzingatia muktadha wa UDSM.

*Inaendelea uk. 17...*

## Mapitio ya mitaala...

*(Inatoka uk. 16)*

"Mambo tuliyojifunza kutoka Chuo Kikuu cha Memphis hususani uhusishwaji wa teknolojia katika mitaala ili kuwashirikisha vilivyo wajifunzaji, ni suala linaloweza kuzingatiwa katika tathmini endelevu", amesema Prof. Killian.

Prof. Saudin Mwakaje ambaye ni Mwanasheria Mkuu wa Chuo na Katibu wa Baraza alibainisha mafunzo waliyoyapata katika ziara yao nchini Ghana. Aidha, Dkt. Egbert E. Mujuni kutoka Ndaki ya Sayansi asilia na tumizi kwa upande wake, alibainisha mafunzo yaliyopatikana wakati wa ziara yao nchini Afrika Kusini.

Wawasilishaji wote wawili walisisitiza umuhimu wa kuwa na mfumo madhubuti wa usimamizi wa masuala ya mitaala.

"Usimamizi madhubuti katika maandalizi ya mitaala utahakikisha kuwa kuna uwajibikaji na ubora ya kitaaluma, mambo ambayo ni muhimu sana katika kuzingatia ubora wa elimu inayotolewa", amesema Prof. Mwakaje

Washiriki wa warsha pia walipata wasaa wa kusikiliza wasilisho kuhusiana na elimu ya fedha ili kuzingatiwa katika mitaala. Wasilisho hili lilitolewa Dkt. Khadija Kishimba kutoka Benki Kuu ya Tanzania.

"Uingizaji wa kipengele cha na elimu ya fedha katika mitaala utawasaidia wanafunzi kuwa na maarifa muhimu na kufanya uamuzi sahihi kuhusiana na masuala ya kifedha. Maarifa haya ni muhimu sana katika ulimwengu tulionao", amesema Dkt. Kishimba.

Katika warsha hii washiriki walitakiwa kuboresha zaidi mitaala yao kwa kuzingatia maoni kutoka katika Kamati ya Kiufundi iliyopitia mitaala hiyo. Prof. Masoud Muruke, Mratibu wa masuala ya mitaala katika Mradi wa HEET UDSM aliwasilisha ripoti hiyo akionesha ubora na udhaifu katika mitaala yetu uliobainika katika mapitio ya awali ya kamati.

"Lengo letu ni kuhakikisha kwamba kila mtaala unaendana na malengo ya elimu ya Chuo huku ukizingatia mahitaji ya msingi ya wajifunzaji", amesema Prof. Muruke.

Dkt. Geradius D. Kikumi na Dkt. Aurelia Kimaro kwa upande wao walisisitiza umuhimu wa mitaala yetu kuzingatia muundo mahususi unaoendana na miongozo ya TCU. Muundo huu unatoa mwongozo unaohakikisha kwamba uandaaji, utekelezaji na tathmini ya mitaala yetu vinafanyika katika mfumo unaofanana na unaozingatia viwango vya kitaifa na kimataifa.

Prof. Joel Mtebe, ambaye ni Rasi wa Ndaki ya Habari na Mawasiliano, alisisitiza umuhimu wa kuzingatia teknolojia za kisasa katika mchakato wa ufunzaji na ujifunzaji. Alieleza kwamba teknolojia siyo tu kwamba inawezesha kutoa fursa kwa wanafunzi kushiriki vilivyo katika mchakato wa ujifunzaji, bali ndiyo msingi katika kufikia malengo ya kuwa na elimu shirikishi na inayoendana na mabadiliko katika jamii.

## Kamati ya MELL ....

*(Inatoka uk. 9)*

HEET. Kamati hii imechaguliwa kwa umakini kulingana na Mpango Mkakati wa Uwekezaji wa Chuo, ili kuhakikisha kuna mchanganyiko wa ujuzi maalum ambao ni muhimu kwa mafanikio ya mradi.

"Wajumbe wanatoka katika idara tofauti. Tuna mtaalamu wa uchumi, Dkt. Rosemary Taylor; Dkt. Siajali Pamba, anayeangazia mazingira na uhandisi; Dkt. Egidius Kamanyi, mwanasosholojia; na Dkt. Josiah Nombo, mtaalamu wa TEHAMA, pamoja na katibu wa kamati, Bi. Ania Dachi, kutoka Kurugenzi ya Mipango, Maendeleo na Uwekezaji. Wote hawa wanachangia katika nyanja tofauti za Mradi', alisema Dkt. Pantaleo.

Alisema kwamba mtaalamu wa uchumi ana jukumu muhimu katika kuzingatia kujenga uwezo na uhusiano wa kitasnia, akihakikisha kwamba maendeleo ya elimu yanaendana na mahitaji ya soko. Mhandisi na mtaalamu wa mazingira wanasimamia miradi ya ujenzi, wakihakikisha inakidhi viwango vya mazingira na malengo endelevu.

"Mwanasosholojia anahakikisha kwamba mradi unashughulikia masuala muhimu ya kijamii, ikijumuisha usawa wa kijinsia na ujumuishwaji wa watu wenye mahitaji maalum ili kutengeneza mazingira ya kujifunza yenye usawa zaidi. Aidha, mtaalamu wa TEHAMA ana jukumu la kusimamia vipengele vya kiteknolojia vya mradi akihakikisha kwamba teknolojia ya kisasa inajumuishwa katika miundombinu ya chuo ili kusaidia uvumbuzi na kujifunza kidijitali", alisema Dkt. Pantaleo.

Dkt. Pantaleo, ambaye ni Mtaalamu wa Ufuatiliaji na Tathmini na Mwenyekiti wa kamati, alisema, "Moja ya masharti muhimu kwa mwenyekiti ni kwamba lazima awe mtaalamu wa ufuatiliaji na tathmini. Kutokuwa na sifa hiyo kunamfanya mtu asifae kuwa Mwenyekiti, hivyo kuhakikisha kwamba wakati wote kamati ina usimamizi wa kitaalamu kwa upande wa tathmini".

Kadri Mradi wa UDSM-HEET unavyoendelea kubadilika, kamati ya MELL inaendelea kuwa nguzo muhimu katika kuhakikisha mafanikio yake. Pamoja na timu yenye taaluma mbalimbali, mfumo wa wazi wa ufuatiliaji, na jitihada endelevu katika uboreshaji, timu hiyo ina nafasi nzuri ya kukisaidia Chuo kufikia malengo yake makubwa chini ya mpango wa HEET.



*Kamati ya Ufuatiliaji, Tathmini na Mafunzo (MELL) katika mradi wa HEET Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ikiwa katika moja ya vikao vyake hivi karibuni*



# Ujenzi wa Majengo ya Mradi wa HEET UDSM Kukamilika kwa Wakati

*By Dotto Kuhenga, UDSM-HEET*

Ujenzi wa majengo 24 ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam yaliyopo Dar es Salaam, Zanzibar, Lindi (Ngongo na Ruangwa) na Kagera unaofadhiliwa na Mradi wa HEET unaendelea vizuri na kuwa utakamilika kwa wakati, imeelezwa.

Kwa mujibu wa taarifa ambazo Timu ya Jarida hili imezipokea wakati ilipofanya ziara katika maeneno ya ujenzi mwezi Septemba 2024, maendeleo ya ujenzi yanatia matumaini ya mradi huu kukamilika kwa wakati.



*Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. William A.L. Anangisye (katikati) alipotembelea eneo ambalo ujenzi wa majengo chini ya mradi wa HEET Chuo Kikuu cha Dar es Salaam unaendelea, mkoani Kagera hivi karibuni. Kulia kwake ni Dkt. Liberato Haule, Naibu Mratibu wa Mradi wa HEET UDSM na kushoto kwake ni Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Milki, Mhandisi Benedict Chilla.*

Akizungumza na waandishi wa Habari hivi karibuni, Naibu Mratibu wa Mradi wa HEET UDSM, Dkt. Liberato Haule, alieleza namna ambavyo UDSM kilivyodhamiria kutekeleza ujenzi na shughuli nyingine za Mradi kwa wakati.

"Tunaridhika na maendeleo ya mradi katika kila eneo na tuna matarajio makubwa kwamba shughuli zote zitakamilika kwa wakati kwani fedha za kufanikisha Mradi huu zipo", amesema Dkt. Haule

Ameendelea kueleza kwamba Chuo kinafuatilia kwa karibu, kinaratibu na kusimamia kwa ufanisi utekelezaji wa mradi. Chuo kimejipanga kuwasimamia kwa umakini wakandarasi na washauri wa kitaalamu ili kuhakikisha kwamba tunakuwa na majengo ya kisasa.

Tarehe 22 Februari 2024 Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilisaini mikataba na wakandarasi wanne kwa ajili ya ujenzi wa majengo 21 kati ya 24 yaliyopangwa kujengwa Dar es Salaam, Zanzibar, Lindi (Ngongo na Ruangwa) na Kagera kupitia Mradi wa HEET.

Aidha, mikataba kwa ajili ya ujenzi wa majengo matatu mkoani Kagera ambao utakamililsha jumla ya majengo 24 yanayofadhiliwa na Mradi wa HEET UDSM ulisainiwa tarehe 17 Mei 2024. Ujenzi huu unahusisha majengo ya utawala na shughuli za kitaaluma, cafeteria, jengo la biashara, na hosteli ya wasichana.

Kwa mujibu wa ziara tuliyoifanya na maelezo ya wakandarasi na wasimamizi wa ujenzi katika majengo haya, maendeleo ya Mradi yamefikia asilimia 12.

***Inaendelea uk. 19...***

# Ujenzi wa Majengo...

*(Inatoka uk. 18)*



## Miradi mbalimbali ya Ujenzi

Kwa mujibu wa Dkt. Paul Ndumbaro, Mtaalamu wa Mradi wa HEET-UDSM kwa upande wa maendeleo ya miundombinu, wakandarasi wanaojenga majengo haya ni pamoja na M/S Mohammed Builders; M/s B.H. Ladwa; M/S Til Construction; and M/s Shandong Hi-Speed. Mikataba yao ni ya miezi 18 kutoka tarehe ya kusainiwa kwa mkataba na kwamba miradi hii inagharimu TZS 45,993,168,271.79.

Mkataba kati ya UDSM na M/S Mohammed Builders unahusisha shughuli za ujenzi katika ndaki mbalimbali katika Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere- Mlimani wenye thamani ya TZS 15,696,130,949,32 ukijumuisha ujenzi wa majengo katika Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia (CoET) wenye thamani ya TZS 9,052,693,573.95 na kiasi cha TZS 6,643,437,375.37; ni kwa ajili ya jengo litakalojengwa baina ya Bweni Na. 6 na ukumbi wa mhadhara wa Yombo pamoja na Jengo la Jinsia na watu wenye mahitaji maalum.

Ujenzi katika Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia unahusisha ukarabati wa Bloku L, O na Q; ujenzi wa jengo jipya linalojumuisha maabara 7; jengo jipya lenye karakana 5; jengo jipya kwa ajili ya ukumbi 1 wa mihadhara (wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 250), vyumba 3 vya mihadhara (kila kimoja kikiwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 50) na chumba 1 cha studio wa kuchukua wanafunzi 50 wa programu ya usanifu vitambaa).

Majengo mengine yanayotarajiwa kujengwa katika Kampasi ya Mwalimu Nyerere ndani ya mkataba huu ni, jengo la jinsia na watu wenye mahitaji maalumu pamoja na hosteli ya wanafunzi wa uzamili yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 51.

Mkataba na M/s B.H. Ladwa, wenye thamani ya TZS 6,459,181,103.97, unahusisha ujenzi wa jengo 1 la mihadhara lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 140; studio 1 ya maltimidia yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 50; maabara 3 za kisasa zitakazokuwa na vifaa vyenye teknolojia ya hali ya juu, kila moja ikiwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 48; na karakana 2, kila moja ikiwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 30 katika Ndaki ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Kijitonyama.

Aidha, kutakuwa na ujenzi wa vyumba 3 vya mihadhara, kila kimoja kikiwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 100 na maabara 1 yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 50 katika Shule ya Kuu ya Sayansi ya Akua na Teknolojia ya Uvuvi iliyopo Kunduchi.

## Ujenzi wa majengo mapya nje ya Dar es Salaam

Miongoni mwa mafanikio makubwa ya Mradi wa HEET ni upanuzi wa Chuo unaohusisha ujenzi majengo majengo mapya nje ya Dar es Salaam.

Taasisi ya Sayansi za Bahari ambayo hadi siku za hivi karibuni imekuwa ikijihusisha zaidi na wanafunzi wa uzamili, imenufaika katika upanuzi wa miundombinu kupitia Mradi wa HEET.

Suala hili linajidhihirisha katika Mkataba kati ya UDSM na M/S Til Construction wenye thamani ya TZS 10,118,405,530.78 unahusisha ujenzi wa majengo mapya 11 yakiwamo ya utawala na taaluma (kwa ajili vyumba vya mihadhara, maabara, ukumbi wa mikutano, ofisi za wafanyakazi na jengo moja jipya la hosteli litakalokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 80) katika Taasisi ya Sayansi za Bahari (IMS) Buyu, Zanzibar.

Ujenzi katika mkoa wa Lindi unatekelezwa katika mkataba kati ya UDSM na M/s Shandong Hi-Speed wenye thamani ya TZS 13,719,450,687.7 unahusisha ujenzi katika maeneo ya Ruangwa na Ngongo mkoani Lindi.

Katika eneo la Ngongo kutajengwa jengo la utawala, jengo la vyumba vya mihadhara (vyenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 360), jengo la maabara, jengo la karakana (vyumba 5), jengo la hosteli za wanafunzi wa kiume na hosteli za wanafunzi wa kike.

Katika eneo la Ruangwa, kutakuwa na ujenzi wa ukumbi wa mihadhara (wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 50) na jengo 1 la hosteli ya wanafunzi 56 (wa kike 22 na wanaume 34).

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pia kilisaini mkataba wenye thamani TZS 13,174,734,974.55 na China Jiangxi Corporation kwa ajili ya ujenzi wa majengo matatu katika Kampasi ya Kagera. Majengo hayo yanahusisha jengo la utawala na taaluma, kafeteria, jengo la biashara, na jengo la hosteli za wasichana.



# UDSM chatoa mafunzo kuhusu Ukatili wa Kijinsia kwa watoa huduma katika maeneo ya HEET

Na Mercy Machange, UDSM-HEET

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimeanzisha mpango muhimu wa kubainisha na kutoa mafunzo ya Ukatili wa Kijinsia kwa watoa huduma katika maeneo mbalimbali ya ujenzi wa Mradi wa HEET UDSM nchini Tanzania.

Mpango huu, ulioanzishwa katika maeneo ya Lindi, Zanzibar, Kagera, na katika kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere Mlimani jijini Dar es Salaam, ni muhimu kwa sababu unatoa mafunzo na kutengeneza mtandao wa watu wenye mafunzo ambao wana jukumu la kusaidia katika mapambano ya ukatili wa kijinsia katika maeneo ya mradi na katika jamii zinazozunguka.

Mratibu wa masuala ya Jinsia wa Mradi wa HEET-UDSM, Dkt. Lulu Mahai, amesema lengo kuu la mpango huu ni kutengeneza mazingira wezeshi ambayo yanazuia na kushughulikia masuala ya ukatili wa kijinsia kwa ufanisi.

"Mbinu hii inahakikisha usalama na ustawi wa watu ndani na kuzunguka maeneo ya ujenzi na kukuza utamaduni wa heshima na utu", amesema Dkt. Mahai.

"Mafunzo kwa watoa huduma kuhusu ukatili wa kijinsia ni hatua muhimu katika kuhakikisha kwamba maeneo yetu ya ujenzi ni salama kwa kila mtu. Watoa huduma kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wanaweza kushughulikia masuala ya ukatili wa kijinsia kwa ufanisi zaidi na kutengeneza mazingira wezeshi zaidi", amesema Dkt. Mahai.

Alisema watoa huduma walioshiriki katika mpango huu ni wale wanaotekeleza jukumu muhimu katika kusimamia na kushughulikia masuala ya ukatili wa kijinsia. Washiriki walijumuisha maofisa polisi wa dawati la jinsia, wenyeviti wa vijiji, maofisa watendaji wa kata, wasimamizi wakuu wa miundombinu katika Mradi wa HEET, wakuu wa shule, maofisa wa maendeleo ya jamii, maofisa jamii katika hospitali, wanajamii maarufu, na Asasi Zisizo za Serikali kama vile Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

Dkt. Mahai aliongeza kuwa mafunzo hayo yalihusisha masuala kama ukatili wa kijinsia, ikijumuisha unyanyasaji wa kingono, udhalilishaji na unyanyasaji miongoni mwa wanafunzi, wafanyakazi, wadau, na watu wenye mahitaji maalum. Pia, yalihusisha mifumo ya kuripoti ukatili wa kijinsia na msaada unaopatikana, pamoja na Mifumo ya Kushughulikia Malalamiko.

"Watoa huduma hawa wamebainishwa kwa umakini na kuhamasishwa kushirikiana ipasavyo na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mafunzo haya yamewapa mbinu za kushughulikia masuala ya ukatili wa kijinsia kwa njia inayofaa ili kuhakikisha mazingira salama na wezeshi", aliongeza.



Ubainishaji na Mafunzo kuhusu Ukatili wa Kijinsia kwa watoa huduma katika maeneo mbalimbali ya ujenzi wa Mradi wa HEET UDSM nchini Tanzania chini ya Mratibu wa masuala ya Jinsia wa Mradi wa HEET-UDSM na Mkurugenzi wa Taasisi ya Jinsia, Dkt. Lulu Mahai (kushoto-aliyesimama).

### Wajibu na Majukumu ya watoa huduma

Kamati za watoa huduma kuhusu ukatili wa kijinsia zimeundwa na kupewa mafunzo ili kuelewa majukumu na mipaka yao. Majukumu yao makuu ni pamoja na kupokea ripoti za masuala ya ukatili wa kijinsia/ udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono(GBV/SEAH) kutoka kwa waathirika, kutunza kumbukumbu ya kesi zilizoripotiwa kwa siri, na kuwasilisha ripoti hizo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa ajili ya kushughulikiwa.

"Watoa huduma hawa pia wanaweza kutoa mwongozo wa kitaalamu kwa Chuo Kikuu kuhusu masuala ya ukatili wa kijinsia na kuwahamasisha wanajamii kuzuia matukio ya ukatili wa kijinsia," amesema Dkt. Mahai.

Watoa huduma walieleza kwamba wamejizatiti kikamilifu kushirikiana ili kuzuia ukatili wa kijinsia na kuwasaidia waathirika. "Mpango huu unatuwezesha si tu sisi bali pia jamii nzima kupinga ukatili wa kijinsia," amesema mmoja wa watoa huduma hao.

Mpango huu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni ushahidi wa umuhimu wa ushirikiano na mafunzo katika kushughulikia masuala muhimu ya kijamii kama ukatili wa kijinsia katika utekelezaji wa Mradi wa HEET.

Kwa kuwawezesha watoa huduma na kukuza utamaduni wa heshima na utoaji msaada, Chuo kinachukua hatua muhimu kuelekea kutengeneza mazingira salama na mustakabali jumuishi zaidi katika maeneo ya ujenzi wa Mradi wa HEET na jamii zinazoizunguka.




Mafunzo kwa wafanyakazi wa utawala na wafanyakazi wapya walioajiriwa hivi karibuni kuhusu muhimu wa kukuza mazingira yasiyo na ukatili wa kijinsia (GBV), yaliyofanyika hivi karibuni katika Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere Mlimani hivi karibuni.

# Jitihada madhubuti za kukuza mazingira yasiyo na ukatili wa kijinsia UDSM zapamba moto

Na Mercy Machange, UDSM-HEET

Katika hatua ya kuhakikisha kunakuwa na mazingira salama na wezeshi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimeendesha mpango wa mafunzo jumuishi kwa wafanyakazi wa utawala na wafanyakazi wapya walioajiriwa hivi karibuni ili kuwapatia ujuzi muhimu wa kukuza mazingira yasiyo na ukatili wa kijinsia (GBV).

Mratibu wa Mradi wa HEET – UDSM na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Mipango, Fedha na Utawala, Prof. Bernadeta Killian, amesema kwenye hafla ya ufunguzi wa mafunzo yaliyofanyika Dar es Salaam kwamba lengo kuu ni kuongezea uelewa kuhusu ukatili wa kijinsia na sera zinazohusiana na masuala ya ukatili wa kijinsia, kuwawezesha wasimamizi kufanya kazi kwa ufanisi ndani ya vitengo vyao, na kuhakikisha utekelezaji sahihi wa sera dhidi ya ukatili wa kijinsia.

"Mpango huu unalenga kuwezesha wasimamizi na watoa huduma ili kuzuia na kushughulikia masuala ya ukatili wa kijinsia kwa ufanisi. Mpango unalenga kutengeneza kundi la mabalozi walio tayari kuzuia na kushughulikia masuala ya ukatili wa kijinsia, hivyo kukuza mazingira wezeshi na salama katika Chuo Kikuu", amesema Prof. Killian.

Prof. Killian alisema kwamba Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kiko mstari wa mbele katika kukuza usawa wa kijinsia na kutokomeza ukatili wa kijinsia, "kama ilivyoelezwa wazi katika Dira yetu ya mwaka 2061 na Sera yetu ya Jinsia ya mwaka 2006, iliyorekebishwa mwaka 2023".

Mpango huu upo ndani ya malengo makuu ya chuo chetu, ambayo ni ufundishaji, utafiti, na huduma kwa jamii. Malengo haya hayawezi kufikiwa kama hatutekelezi majukumu yetu kwa uaminifu na kuepuka ukatili wa kijinsia", amesema.

Awali, Mratibu wa Masuala ya Jinsia katika Mradi wa HEET-UDSM na Mkurugenzi wa Taasisi ya Jinsia, Dkt. Lulu Mahai alisema kwamba mafunzo hayo yalijumuisha masuala yanayohusiana kama jinsia na ukatili wa kijinsia, ikijumuisha udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono, mifumo ya kuripoti ukatili wa kijinsia, na msaada unaopatikana kwa masuala ya maadili na jinsia katika kanuni za maadili za UDSM, pamoja na sera na miongozo inayohusiana na jinsia.

"Mafunzo haya yametupa mwanga kuuelewa vilivyo ukatili wa kijinsia na namna ya kuushughulikia ndani ya jamii yetu ya chuo. Sasa tuna zana na maarifa ya kutengeneza mazingira ya kazi salama na wezeshi kwa kila mtu", alisema mmoja wa washiriki wa mafunzo.





# Kampasi mpya ya UDSM yachochea uwekezaji Mkoa wa Kagera

*Na Jacob Mosenda*



*Eneo ambalo ujenzi wa majengo ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kupitia mradi wa HEET unaendelea kwa ajili ya Kampasi ya Kagera. Hii ilikuwa mnamo mwezi Septemba, 2024.*

Mkoa wa Kagera unashuhudia mageuzi makubwa ambapo wafanyabiashara wengi wameanza kukimbilia fursa ya uwekezaji karibu na Kampasi ya Shule Kuu ya Biashara ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Maendeleo haya yamefungua fursa kwa wawekezaji kutoka ndani na nje ya Mkoa wa Kagera wanaotamani kuitumia fursa ya biashara inayotokana na ujenzi wa kampasi hii.

Kampasi hii yenye ukubwa wa hekta 315 ambayo iko takriban kilomita 15 kutoka Bukoba mjini inaweka alama ya matumaini na ustawi wa wakazi wa mkoa wa Kagera.

Mradi huu utakaogharimu ShT bilioni 13 ni sehemu ya Mradi wa HEET unaofadhiliwa na Benki ya Dunia umekuwa kichocheo kwa maendeleo katika mkoa huu.

Wakati ujenzi wa kampasi hii kiendelea, thamani ya ardhi katika eneo la mradi imepanda na wakazi wa eneo hilo wameanza kunufaika kutokana na mradi huu.

“Nimeuza sehemu ya shamba langu kwa ShT milioni 25”, ameeleza ndugu Emmanuel Byemelwa mkazi wa Kata ya Karabagaine ambapo kampasi hii inajengwa.

“Watu wanavutiwa sana na fursa hii. Fursa hii siyo tu kwamba itatokana na uuzaji wa ardhi, bali itakuwa ni chachu kwa mabadiliko ya kiuchumi kwa mkoa wote wa Kagera”, ameendelea kueleza Bw. Byemelwa.

Kwa muda mrefu mkoa wa Kagera umekuwa ukisifika kwa kuzalisha wasomi lukuki, lakini wasomi hawa wamekuwa wakitoka kutafuta fursa za uwekezaji katika elimu ya juu nje ya mkoa wa Kagera.

Uanzishwaji wa Kampasi ya Shule Kuu ya Biashara ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika mkoa wa Kagera unatoa fursa ya kuwarejesha wasomi hawa na kuwavutia zaidi wawekezaji kutoka maeneo ya jirani ikiwa ni pamoja na Uganda kuwekeza katika mkoa huu.

“Mwanangu amekuwa akiishi Dar es Salaam kwa karibu miaka 20 sasa, lakini aliposikia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinajenga kampasi katika vijiji vya Itahwa na Kangabusharo ameamua kurejea mkoani Kagera”, amesema mzee Yusufu Mkure, mkazi wa Muleba.

Uwekezaji mkubwa kuzunguka eneo la mradi unaashiria mabadiliko makubwa ya kiuchumi katika eneo hili.

Kampasi hii inatarajiwa kuwa kichocheo cha ukuaji wa biashara na kuzalisha ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja kwa wakazi wa mkoa huu.

Wawekezaji wanaotazama mbali, wananunua ardhi kuzunguka eneo la mradi kwa matarajio ya ongezeko la mahitaji ya huduma mbalimbali kama hosteli na maduka ya rejareja.

“Tunatarajia kuwa na mzunguko wa fedha kwa mabilioni ya shilingi kutokana na mradi huu”, ameeleza Bw. Thomas Makori, mchumi kutoka Bukoba.

“Bei ya ardhi imepanda hadi kufikia ShT milioni 30 kwa hekari moja kwa baadhi ya maeneo”, ameendelea kueleza Bw. Makori.

Ujenzi wa Kampasi ya Kagera ya sehemu ya utekelezaji wa Mradi mkubwa wa HEET unalenga kuimarisha elimu ya juu nchini Tanzania na kuboresha mitaala ili kuendana na mahitaji ya sasa ya soko la ajira.

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambacho ni chuo kikongwe na kikubwa nchini Tanzania, kimepata Dola za Kimarekani

***Inaendelea uk. 23...***

# Kampasi mpya...

(Inatoka uk. 22)

milioni 47.5 kati ya fedha zote za Mradi wa HEET ambazo ni Dola za Kimarekani milioni 425.

Fedha hizi zitawezesha kuanzishwa kwa kampasi mpya katika mikoa ya Kagera na Lindi pamoja na kuboresha miundombinu katika kampasi za Mlimani zilizopo Dar es Salaam na Taasisi ya Sayansi za Bahari, Zanzibar.

Ujenzi wa kampasi hii mkoani Kagera unatarajiwa kuleta mabadiliko makubwa katika mkoa huu zaidi ya miundombinu inayojengwa.

Kihistoria licha ya mkoa wa Kagera kuwa na ardhi yenye kuvutia na mazingira rafiki kwa miundombinu ya kielimu, mkoa huu umesahaulika kwa muda mrefu katika miundombinu ya elimu ya juu.

“Chuo hiki kitakuwa ni kichocheo muhimu kwa wananchi wetu kuendelea kuwekeza katika elimu”, amesisitiza Mhe. Samwel Makwabe ambaye ni Diwani wa Kata ya Karabagaine.

Watoto wetu hawatakuwa na sababu ya kusafiri umbali mrefu kwa ajili ya elimu ya juu, bali wanaweza kusoma hapahapa.”

Kampasi hii inayotarajiwa kuwa na wanafunzi 10,000 katika kipindi cha miaka kumi ijayo, itakuwa ni mahususi kwa masomo ya Biashara na Ujasiriamali.

Kuna mpango pia wa kufungua kituo cha ujasiriamali katika kampasi hii ambacho kitakuwa msaada kwa maendeleo ya wafanyabiashara wadogo.

“Tunatarajia kuileta miundombinu ya elimu ya juu karibu na jamii ambayo kwa muda mrefu haikupewa fursa hii”, Amesema Dkt. Liberato Haule, Naibu Mratibu wa HEET UDSM.

“Kampasi ya Kagera ni sehemu ya mikakati yetu ya kuongeza kiwango cha udahili ili kuhakikisha kwamba Watanzania wengi zaidi wanapata fursa ya elimu ya juu”, amesema Dkt. Haule.



*Afisa Mipango wa Wilaya ya Bukoba mjini, Bw. Bruno Barongo akiongea na Waandishi wa Habari mwezi Septamba, 2024 katika eneo ambalo ujenzi wa majengo ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kupitia mradi wa HEET unaendelea mkoani Kagera.*

Kwa sasa UDSM inapokea maombi zaidi ya 60,000 kwa mwaka kwa programu za shahada ya awali lakini kutokana na changamoto ya miundombinu na ikama ni takriban 10% ya waombaji hao ndio hudahiliwa.

Kampasi hizi mpya zitasaidia kupunguza changamoto hii kwa kukiwezesha chuo kuongeza kiwango cha udahili kama ilivyo kwa vyuo vya nchi za jirani kama vile Kenya.

Wakati ujenzi wa kampasi hii ukiendelea, viongozi wa maeneo haya wana matumaini makubwa kwamba kampasi hii itauinua sana mkoa huu.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Itahwa Bw. Philemon Anatory ameeleza namna ambavyo wananchi wa Kagera wamekuwa wakitumia fedha nyingi kuwasomesha watoto wao nje ya mkoa huo.

“Tumekuwa tukilipa fedha nyingi kuwasomesha watoto wetu nje ya mkoa”, amesema Bw. Anatory.

“Nimekuwa nikitumia gharama kubwa kuwasomesha watoto wangu nchini Uganda. Kuwapo kwa Kampasi hii hapa kutatuokolea fedha nyingi wakazi wa mkoa huu ambazo tumekuwa tukizitumia kuwasomeshea watoto wetu.”

Kampasi hii siyo tu kwamba itawanufaisha wakazi wa Kagera, wawekezaji kutoka Uganda pia watanufaika na kuwapo kwa kampasi hii. Hivyo, fursa ya kuwapo kwa kampasi hii itavuka mipaka ya mkoa wa Kagera.

Mradi huu utakaohusisha ujenzi wa madarasa, kumbi za mihadhara, mabweni na ofisi mbalimbali unatarajiwa kukamilika ifikapo mwaka 2025.

“Huu ni mwanzo tu, tumekwishatenga eneo zaidi kwa ajili ya uwekezaji huu, Kamapsi hii itabadili mandhari ya mkoa wa Kagera”, amesema Afisa Mipango wa Bukoba mjini, Bw. Bruno Barongo.

Mradi huu unatoa fursa mpya kwa mkoa wa Kagera na kuufanya mkoa huu kuwa kitovu cha elimu, ujasiriamali na ukuaji wa uchumi.

Ujenzi wa kampasi hii utakapokamilika, unatarajiwa kufungua fursa nyingi katika mkoa huu.

***Makala hii imechapishwa kwa mara ya kwanza katika gazeti la The Citizen la tarehe 2 Oktoba 2024.***



*Meneja wa Mradi, Bw. Huang Dang, akiongea na Waandishi wa Habari hivi karibuni katika eneo ambalo ujenzi wa majengo ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kupitia mradi wa HEET unaendelea mkoani Kagera.*

# UDSM chapongezwa kwa kuzindua kamati za KASEMA katika maeneo ya Mradi wa HEET

Na Dotto Kuhenga, HEET-UDSM



*Naibu Mratibu wa Mradi wa HEET, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Dkt. Liberato Haule (kushoto), Diwani wa Kata ya Chukweni, na Dkt. Daudi Msangameno (wa pili kulia) akimwakilisha Mkurugenzi wa Taasisi ya Sayansi za Bahari (IMS), wakikabidhi vitendea kazi kwa Katibu wa kamati ya Mfumo wa Kushughulikia Maoni na Malalamiko (GRM) inayojulikana kama KASEMA, wa IMS, Zanzibar.*



*Naibu Makamu Mkuu wa Chuo-Mipango, Fedha na Utawala na Mratibu wa Mradi wa HEET, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof. Bernadeta Killian (katikati) na viongozi wa Wilaya ya Lindi, wakikabidhi vitendea kazi kwa Katibu wa kamati ya Mfumo wa Kushughulikia Maoni na Malalamiko (GRM) inayojulikana kama KASEMA, katika eneo la Ngongo, Mkoa wa Lindi.*

Wakazi katika maeneo ambapo majengo ya UDSM yaliyo chini ya Mradi wa HEET yanajengwa wamekipongeza Chuo kwa kuanzisha na kuzindua kamati za Mfumo wa Kushughulikia Maoni na Malalamiko (GRM) zinazojulikana kama KASEMA.

Wakizungumza wakati wa uzinduzi wa KASEMA katika maeneo ya Dar es Salaam, Lindi, Zanzibar, na Kagera, wakazi hao, wakiwamo viongozi wa mitaa, walisema kwamba kamati hizi ni muhimu sana kwa sababu zitapokea na kushughulikia matatizo ya wananchi ili kuboresha utekelezaji wa mradi.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, Bw. Andrew Chikongwe, alikipongeza UDSM kwa kuzindua kamati muhimu kama hizo na kuahidi kwamba wakazi wa Ruangwa, ambapo Kituo cha Utafiti kinajengwa, watafanya kazi kwa karibu na wakandarasi kuhakikisha kwamba mradi unatekelezwa kikamilifu.

Prof. Bernadeta Killian, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Mipango, Fedha na Utawala na Mratibu wa Mradi wa HEET-UDSM, aliwataka wakazi katika maeneo yanayohusika kuitumia vizuri KASEMA, ambayo inajumuisha viongozi wa mitaa na wakazi, ili kutoa mapendekezo zaidi ya kuboresha utekelezaji wa mradi.

"Chuo kinachukulia KASEMA kama vyombo muhimu vya ushirikishwaji wa wadau katika utekelezaji wa Mradi wa HEET. KASEMA zitumiwe ipaswavyo na kwa hekima ili kuhakikisha kwamba ujenzi na shughuli nyingine za mradi zinafanyika kwa urahisi, kulingana na mipango na malengo", amesema Prof. Killian.

Wakati huohuo, Mtaalamu wa Maendeleo ya Kijamii wa Mradi wa HEET- UDSM, Dkt. Jacqueline Mgumia, alielezea mchakato uliopitiwa kuunda kamati za mfumo wa kushughulikia malalamiko ya mradi, KASEMA, na hatimaye kuzinduliwa rasmi katika maeneo yanayohusika.

"Kwanza, ulianza mchakato wa kuandaa zana na mwongozo; hatua hii ilifuatwa na kuunda kamati katika maeneo yanayohusika, kisha kufanya mafunzo husani kuhusu zana za kazi na majukumu ya Kamati (KASEMA)," alielezea Dkt. Mgumia.

Dkt. Mgumia alisema kwamba baada ya mchakato huo wa awali, uzinduzi ulifanyika ambapo kamati zilithibitishwa rasmi kutekeleza shughuli zao kulingana na ratiba ya mradi. "Kwa ujumla, huu ni mchakato wa mfumo wa kushughulikia malalamiko kwa ajili ya kupokea, kutathmini, na kushughulikia malalamiko na maoni yanayohusiana na mradi kutoka kwa wadau".

Alisema kwamba mradi ulianzisha mfumo huo tangu mwezi Februari/Machi 2024, lakini wanakamati hawakuwa na ujuzi mzuri wa namna ya kushughulikia matatizo/malalamiko hatua kwa hatua. Hivyo, mafunzo yamesaidia kamati kuelewa "mchakato wa ushughulikiaji" ambapo utawezesha malalamiko kushughulikiwa na kutatuliwa kwa urahisi.

Mafunzo yalijikita katika taratibu tano ambazo ni kupokea, kuchambua, na kuandikisha; kuchunguza taarifa kwa kina; kuarifu, kuchakata au kupitia; kuchunguza na kutatua; na kufunga au kukata rufaa," alieleza.

Dkt. Mgumia aliongeza kwamba katika uzinduzi wa KASEMA, wanachama walifafanuliwa kuhusu muktadha wa Mradi wa HEET kitaifa, hususani kuhusu malengo ya serikali ya kueneza maarifa ya kiwango cha juu yatakayochangia katika mabadiliko ya kiuchumi ya nchi.

"Walielezwa pia kuhusu masharti ya mkopo wa Benki ya Dunia kuhusiana na Mradi wa HEET na sababu za umuhimu wa Mfumo wa Kushughulikia Malalamiko katika mradi huo. Malengo ya Mfumo wa Kushughulikia Maoni na Malalamiko yalifafanuliwa na wanakamati walikumbushwa kufuata vigezo vya maadili na majukumu vilivyoainishwa katika mwongozo wa mafunzo", aliongeza.

Katika hafla za uzinduzi, zilizohudhuriwa na maofisa wa serikali za mitaa, wanakamati wa KASEMA na maofisa wa Mradi wa UDSM-HEET, kulikuwa na jumla ya washiriki 131 waliohudhuria kutoka maeneo yote.

"Kati ya washiriki hao, Dar es Salaam walikuwa 33, Zanzibar 20, Kagera 22, Ruangwa 32, na Ngongo 24. Katika eneo la Dar es Salaam, uzinduzi ulijumuisha kamati tatu kutoka maeneo ya Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere Mlimani, Chuo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na Shule Kuu ya Sayansi Akua na Teknolojia ya Uvuvi", alisema.



**Bw. Nelson Kimaro**
Mhitimu wa Shahada ya Umahiri ya Sayansi katika Uhandisi wa Umeme, Chuo Kikuu cha Essex, Uingereza.



**Mhandisi Delain Mwakalasi**
Mhitimu wa Shahada ya Umahiri ya Sayansi katika Uhandisi wa Umeme na Nishati Mbadala, Chuo Kikuu cha Leeds, Uingereza.



**Mhandisi William Mnozya**
Mhitimu wa Shahada ya Umahiri ya Sayansi katika Uhandisi wa Miundo, Chuo Kikuu cha Leeds, Uingereza.

# Wanufaika wengine watatu wa Ufadhili wa HEET UDSM wahitimu Masomo ya Umahiri

*Na Ally Mambele, HEET- UDSM*

Wanataaluma watatu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambao ni miongoni mwa wanufaika wa ufadhili unaotolewa kupitia Mradi wa HEET UDSM wamehitimu masomo yao ya Umahiri. Imeripotiwa katika Jarida hili

Wanataaluma hao ni Mhandisi William Mnozya, mkufunzi msaidizi kutoka Idara ya Uhandisi Mihimili na Ujenzi, Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia, Mhandisi Delain Mwakalasi, mhadhiri msaidizi kutoka Idara ya Uhandisi Umeme pia kutoka Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia na ndugu Nelson Kimaro kutoka Ndaki ya Habari na Mawasiliano

Wahitimu wote watatu wamesoma nchini Uingereza ambapo Mhandisi Mwakalasi alisoma Digrii ya Umahiri wa Sayansi katika Uhandisi Umeme na Nishati jadidifu na mhandisi Mnozya alisoma Digrii ya Umahiri wa Sayansi katika Uhandisi Mihimili wote kutoka Chuo Kikuu cha Leeds. Mhandisi Kimaro alihitimu Digrii ya Umahiri wa Sayansi katika Uhandisi umeme kutoka Chuo Kikuu cha Essex.

Wahitimu hawa wanaungana na wanufaika wengine wa ufadhili wa masomo kupitia Mradi wa HEET kusoma Didrii ya Umahiri mwishoni mwa mwaka 2023 na mwanzoni mwa mwaka 2024 mtawalia. Idadi ya wahitimu walionufaika na ufadhili huu sasa wamefikia wanane.

“Ufadhili huu ni sehemu ya bajeti ya USD 200,000 iliyotengwa na UDSM kwa ajili ya ufadhili wa mafunzo ya muda mrefu kupitia Mradi wa HEET na tunafurahi kutoa taarifa kwamba kufikia sasa jumla ya wanataaluma wanane wamehitimu masomo yao kupitia ufadhili huo”, amesema Dkt. Stephen Matei, Mratibu wa HEET kwa upande wa kujenga uwezo.

Kwa mujibu wa Dkt. Matei wanataaluma hawa watatu ni miongoni mwa wanataaluma kumi wa UDSM waliojisajili katika masomo ya Digrii ya Umahiri chini ya ufadhili wa mradi wa HEET-UDSM. “Tunafurahi kuripoti kwamba kufikia mwezi Septemba 2024 jumla ya wahitimu wanane kati ya kumi chini ya ufadhili kutoka Mradi wa HEET wamehitimu masomo yao kwa ufanisi”.

Dkt. Matei ameendelea kueleza kwamba kwa upande wa ufadhili kupitia Mradi wa HEET, UDSM kimevuka lengo kwa kusomesha wanataaluma 23 kati ya 22 waliopangwa kusomeshwa ambapo 10 ni wa shahada ya umahiri na 13 ni kwa upande wa shahada ya uzamivu.

## Wanufaika ufadhili katika Programu ya MSC Wahitimu mwaka 2023 na Machi 2024

Mnamo mwezi Novemba 2023, Jarida hili liliripoti kwamba wanataaluma wanne waliokuwa wamejisajili katika masomo ya umahiri nje ya nchi kwa ufadhili wa Mradi wa HEET walihitimu masomo yao na kurejea kazini. Wanataaluma hawa wanne wanatoka Ndaki ya Kilimo na Teknolojia ya Uvuvi pamoja na Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia. Wanataaluma hao ni Bi. Angelina William Mwakosya, Bi. Salma Damla, Bw. Gabriel Mwaijande Paul na Bi. Mariam Madundo.

Bi. Angelina William, Mkufunzi Msaidizi, kutoka Idara ya Sayansi ya Chakula katika Ndaki ya Kilimo na Teknolojia ya Chakula, CoAF, alipata ufadhili wa HEET mwezi Julai, 2022 kwa ajili ya masomo ya umahiri katika Sayansi ya Chakula katika Chuo Kikuu cha Reading, Uingereza. Bi. Angelina William alitoa shukrani zake za dhati kwa fursa adhimu aliyopatiwa kupitia Mradi wa HEET.

Mfanyakazi mwingine ni Bi. Salma Damla, Mkufunzi Msaidizi kutoka Idara ya Sayansi ya Chakula, Ndaki ya Kilimo na Teknolojia ya Chakula. Bi. Salma Damla aliyekamilisha shahada ya umahiri katika Chuo Kikuu cha Leeds, Uingereza, pia alitoa shukrani zake za dhati kwa fursa hiyo adhimu aliyopatiwa.

Wengine ni: Bw. Gabriel Mwaijande Paul, kutoka Idara ya Uhandisi wa Usafirishaji na Jiotekniki na Uhandisi wa Kijiolojia, Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia, ambaye alimaliza shahada yake ya umahiri katika Uhandisi Jiotekniki kutoka katika Chuo Kikuu cha Leeds, Uingereza na Bi. Mariam Madundo, kutoka Idara ya Uhandisi Mihimili na Ujenzi, Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia ambao nao walishukuru kwa ufadhili huo.

Aidha, mwezi Machi 2024 mnufaika mwingine Bw. Vicent Faustine kutoka Idara ya Uhandisi Kilimo, Ndaki ya Kilimo na Teknolojia ya Uvuvi alihitimu Digrii ya Umahiri wa Sayansi katika Mustakali wa Uendelevu wa Chakula kutoka Chuo Kikuu cha Cranfield, Uingereza.

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

HEET
HIGHER EDUCATION FOR ECONOMIC TRANSFORMATION

## Mawasiliano


Naibu Mratibu: +255 765 939 958

Mhariri Mkuu: +255 755 172 570

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam,
Jengo la Cranford Pratt,
Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere, Mlimani
Barabara ya Chuo Kikuu, 16103 Ubungo
S.L.P. 35091
Dar es Salaam, Tanzania

heet@udsm.ac.tz Heet Udsm www.udsm.ac.tz